



EAST AFRICAN
**CRUDE OIL
PIPELINE**

OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA KIBENKI NCHINI TANZANIA KUMBUKUMBU NA: 10007186

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma za kibenki katika mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:

Kampuni inahitaji kufungua akaunti za benki katika benki mbili za nchini Tanzania. Akaunti zitatumika kwa matumizi ya malipo ya ndani peke yake kupitia mfumo wa kuhamisha fedha kielektroniki. Malipo yatafanyika katika fedha za Kimarekani (USD) na Shilingi za kitanzania (TZS), kwa watoa huduma wengine, mamlaka za ndani pamoja na waajiriwa.

Huduma hizi hazijumuishi malipo ya nje ya mipaka ya Nchi, fedha ngumu kwa ajili ya matumizi ya dharura (Petty cash), kutoa fedha kuzidi kiwango kilichomo, mkopo, kuweka fedha, na maswala mengine ya kifedha.

Pamoja na orodha ya gharama zitakazowasilishwa na benki, watoa huduma wa ndani ndio watakaohitajika, idadi ya matawi, ushindani kwenye kubadili fedha za kigeni, usaidizi wa maswala ya kiuchumi, usaidizi katika huduma, muda wa kikomo wa siku na muda wa kukamilisha mchakato wa kazi, uwezo wa kuhudumu ndani ya tarahie iliyooombwa kwa ajili ya kufanya malipo pamoja na nafasi ya benki katika soko. Na pia utayari wa benki kushiriki katika kuwekeza fedha katika deni la nje linalotarajiwa la kibiasara.

VIGezo MUHIMU:

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Uthibitisho wa Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika mawanda ya kazi.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Inashauriwa, muoneesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoarodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa eacoptz.eoi.1000001@totalenergies.com (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **2nd Desemba 2021**. Kichwa cha Habari cha barua pepe kiwe ni kumbukumbu namba husika tu. Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni **10007186**.

Muhimu: Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.